# CHUO KIKUU CHA DAR ES SALAAM

## MPANGO WA UTAFITI NA ELIMU YA DEMOKRASIA TANZANIA

## (REDET)

## Warsha ya Viongozi Mashuhuri

# Mambo Muhimu ya Demokrasia na Ushirikishwaji wa Raia

**Na**

**Prof. Amon E. Chaligha**

Mada hii ilitolewa kwenye Warsha ya Viongozi Mashuhuri iliyofanyika tarehe 15 Januari 2003 ESRF Dar es Salaam

# MAMBO MUHIMU YA DEMOKRASIA NA USHIRIKISHWAJI WA RAIA
**(Muhtasari wa Mazungumzo)**

Na Amon E. Chaligha, Idara ya Siasa na Utawala, Chuo Kikuu cha Dar es Salaam.

## Utangulizi

Watanzania kwa ujumla wao wameshasikia mambo mengi kuhusu Demokrasia. Kwa watu walio wengi Demokrasia huwa na maana tofauti. Wengine husema Demokrasia ni jambo jema na muhimu katika maisha ya mwanadamu. Wengine hudiriki kusema Demokrasia itakuwa na maana pale tu itakapomwezesha mwananchi kuishi maisha bora. Hapa maisha bora ni pamoja na kuweza kupata mahali pazuri pa kulala, chakula cha kila siku, kusomesha watoto na kuwapatia tiba ya uhakika pindi ikihitajika. Haya ni mambo ya kupata mkate (riziki ) wa kila siku. Wala hatuzungumzii kupata siagi ya kupaka kwenye mkate, kwani hii itakuwa ni anasa kwa walio wengi.

Pamoja na kuwa na uhakika wa kuishi, pia kwa walio wengi Demokrasia itakuwa na maana kama wananchi watashirikishwa kutoa maoni katika maamuzi yatakayogusa maisha yao. Katika Demokrasia ya kweli wananchi hawana budi kushirikishwa, katika utungaji wa sera na utekelezaji wake, katika kuandaa itikadi za vyama vya siasa, katika kuchagua viongozi wanaowataka na kadhalika. Katika muhtasari huu wa mazungumzo tutaelezea kwa kifupi juu ya mambo muhimu katika Demokrasia, pamoja na ushirikishwaji wa jamiii katika mustakabali wa demokrasia nchini Tanzania.

## Mambo muhimu katika Demokrasia

Kama tulivyoainisha kwenye utangulizi, Demokrasia ina maana tofauti kwa watu mbalimbali. Pengine tukubaliane kwamba Demokrasia ni kitu ambacho watu wako tayari kukipigania hata wengine wakiwa tayari kupoteza maisha yao kwa ajili yake. Hivyo basi Demokrasia ina umuhimu wa pekee katika jamii. Wananchi wanapopigania uhuru, siyo nia yao kupata bendera ya taifa pekee, bali wanapigania haki za msingi ambazo kimsingi ndizo huamua hatma ya maisha yao. Uhuru wa kuabudu, uhuru wa kujumuika pamoja na kuunda vyama vya siasa, uhuru wa vyombo vya habari na haki ya kupata habari, na kadhalika kama mada ya haki za Msingi za Binadamu ilivyozumzia.

Jambo la msingi kabisa katika Demokrasia ni kuelewa na kukubali kwamba katika Demokrasia wananchi wenyewe ndiyo walio na kauli ya mwisho nini kifanyike katika nchi yao. Hivyo basi Demokrasia katika Misingi hii ina maana ya haki ya raia katika ushawishi wa kufikia maamuzi yenye kuathiri maslahi yao katika ujumla wake. Hili ni pamoja na kuainisha haki na wajibu wa kila raia. Tuseme kuwa Demokrasia itakuwa na maana pale tu inapokuwa sehemu ya maisha ya kila raia ambapo sauti ya wengi itaamua na wakati huo huo kilio cha wachache kikitiliwa maanani.

**Baadhi ya Misingi ya Demokrasia**

- **Katiba Inayokubalika**

Ili Demokrasia iweze kujengeka na kudumishwa ni lazima iwepo katiba inayokubalika kwa wananci walio wengi. Katiba hiyo haina budi kuainisha vizuri na kwa uwazi kabisa haki,majukumu na wajibu wa raia katika ujenzi wan nchi. Pia katiba sharti ielezee na kuweka bayana mashirikiano kati ya mihimili mitatu ya dola, yaani Tawi la Utendaji (Executive Branch), Bunge (Legislature) na Mahakama (Judiciary). Mgawanyo wa mamlaka (separation of powers) pamoja na uthibiti na urari (checks and balances) wa madaraka kati ya mihimili ya dola ni muhimu iwekwe bayana katika katiba ili kuondosha uwezekano wan chi kuendeshwa kidikteta.

Hapa Tanzania, mgawanyo wa mamlaka kati ya mihimili haujakamilika ipasavyo. Katiba imejaribu kupambanua mgawanyo huu lakini mfumo chotara wa siasa tulio nao, yaani mfumo wa kuchanganya Rais Mtendaji na Waziri Mkuu pamoja na Baraza lake la Mawaziri kutoka Bungeni hupunguza na kuaathiri uwezo wa Bunge kudhibiti tawi la Utendaji. Ili kuweze kutenganisha kabisa mamlaka hizi, ungelifikiwa uwezekano wa kupata Mawaziri wasiotokana na Bunge ili kuondoa uwezekano wa kulindana kama ilivyo sasa.

Katiba haina budi pia kuweka bayana mipaka kati ya ngazi mbalimbali za Serikali. Yaani, mgawanyo wa majukumu, mipaka ya utendaji, wajibu na taratibu za mashirikiano kati ya Serikali Kuu na Serikali za Mitaa ni lazima yatambulike na yawekwe wazi kikatiba. Hali ilivyo sasa hivi, Serikali zetu za Mitaa zinaonekana tu kama

wakala wa serikali kuu, badala ya kuwa serikali za wananchi katika maeneo husika. Hali hii huleka mikanganyiko na migongano na migogoro hasa pale inapotokea kwamba Halmashauri Fulani imeshikwa na madiwani kutoka vyama visivyokuwa madarakani.

Kubwa zaidi hata hivyo, ni kwamba kutokana na katiba iliyoko kutoa mamlaka mlango wa mbele na kuyaachia kwa malango wa nyuma (katiba inatambua kuweko kwa serikali za mitaa na kugawa majukumu, lakini ikaweka kifungu kinachozilazimisha kusimamiwa na kuongozwa na serikali kuu kwa upande mwingine. Jambo hili huzifanya serikali za mitaa kukosa vyanzo vizuri vya mapato, kukosa mamlaka na hadhi ya kuitwa serikali, yaani kukosa uwezo wake yenyewe wa kuamua kwani lazima karibu kila jambo lirejeshwe serikali kuu kwa maamuzi ya mwisho.

Hakuna mtu anayejua Serikali za Mitaa zinaanzia na kuishia wapi (mipaka ya madaraka haieleweki kikatiba). Tuchukue mfano mdogo tu wa Katibu Tarafa. Ngazi hii ni ya chini kabisa katika serikali kuu, kwani katibu Tarafa huajiriwa na huripoti kwa Mkuu wa Wilaya. Lakini baadhi ya Halmashauri zinalalamika kupata maagizo kutoka Serikali Kuu yanayowataka Wakurugenzi wa Halmashauri kuwaalika Makatibu Tarafa kwenye vikao vya Halmashauri (bila shaka na kuwalipia posho?). Utungaji wa sheria ndogo ndogo pia lazima uidhinishwe na Waziri wa Serikali kuu. Bajeti ya Halmashauri sharti kwanza ipitiwe na uongozi wa Mkuu wa Mkoa (Serikali Kuu),kabla ya kuwasilishwa kwenye vikao vya Halmashauri ili kuidhinishwa. Ipo mifano mingi ambayo hudhihirisha ni kwa kiwango gani Serikali Kuu huingilia serikali za mitaa.

Katika kuingiliwa kwa Serikali za Mitaa na Serikali Kuu, Demokrasia huwa dhaifu kwa kukosa uhai wa wadau husika, yaani wananchi katika maeneo yao. Jambo hili hufanywa kuwa gumu zaidi kwa kukosekana kwa chombo mahsusi kilichopewa mamlaka ya kutatatua migogoro na migongano kati ya serikali kuu na serikali za mitaa. Hivyo basi ni muhimu kuitekeleza katiba iliyopo kwa kuunda Mahakama ya Katiba kwa minajili ya kusaidia katika kutatua utata unaojitokeza katika kila mamlaka na katika kila ngazi ya serikali wakati wa kutekeleza majukumu na wajibu wake.

Katiba pia ni lazima iweze kutoa mwongozo wa namna ya kutekeleza Demokrasia ya uwakilishi. Hapa ieleweke kwamba Demokrasia ya uwakilishi inajengwa kwa Misingi ya mambo yafuatayo:

(i) Madaraka na Mamlaka yote sharti yawekwe mikononi mwa wananchi kupitia kwa wawakilishi wao (wabunge, madiwani);

(ii) Uongozi sharti uchaguliwe mara kwa mara kupitia uchaguzi wenye ushindani kamili;

(iii) Wananchi wote wenye sifa ya kupiga kura budi wahamasishwe kujiandikisha na kasha kupiga kura bila vikwazo wala vishawishi;

(iv) Uhuru wa kujumuika hauna budi kutolewa na kulindwa na katiba;

(v) Uhuru wa vyombo vya habari na uhuru wa kutoa na kupata habari shariti pia utolewe na ulindwe na katiba;

(vi) Uhuru wa kuabudu nao budi utolewe na kulindwa na katiba;

(vii) Haki ya kumiliki raslimali nayo pia itolewe na kulindwa na katiba;

(viii) Haki ya maisha bora (quality life) ni muhimu kulindwa na katiba, (yaani kila raia sharti ahakikishiwe kupata huduma muhimu katika maisha yake).

- **Ushindani wa Kisiasa**

Ushindani wa kisiasa ni nguzo muhimu katika ujenzi wa Demokrasia. Mara nyingi ushindani hufanyika kupitia vyama vya siasa katika chaguzi mbalimbali. Hata Katiba yetu inapambanisha watu walioteuliwa na vyama vilivyo na usajili kamili wakati wa uchaguzi. Ushindani huu unahitaji kuboreshwa kwa kuhakikisha yafuatayo:

(i) Uteuzi wa wagombea ndani ya vyama vya siasa ufanyike katika taratibu zilizokubaliwa na wanachama wote;

(ii) Taratibu za uteuzi ziwe wazi;

(iii) Viongozi wawajibike kwa wapiga kura wao siyo kwa mabosi wa vyama;

(iv) Vyama viwe na dira iliyojikita katika itikadi pia sera ambazo wananchi wanaweza kuchagua mbadala;

(v) Uchaguzi kwa ujumla ufanyike kwa uwazi, uhuru na kwa haki;

- Utawala Bora

Demokrasia inaweza kukua na kushamiri pale ambapo serikali iliyo madarakani inaheshimu utawala wa sheria. Jambo hili linawezekana pale ambapo serikali imewawezesha wananchi kuhoji utendaji wake ili waweze kuridhika na kile inachokifanya serikali yao. Maana yake ni kwamba raia ni lazima wawapatiwe elimu ya uraia itakayowawezesha kubaini pale haki zao za msingi zinapopokonywa na viongozi waliowachagua wenyewe. Raia asiyejua haki zake hawezi pia kupambanua wajibu na majukumu yake katika ujenzi wa Demokrasia imara. Pia raia wa namna hiyohawezi kusisitiza utawala wa sheria kwani atakuwa haijui sheria mama (katiba) wala sheria zitokanazo na katiba hiyo.

Kwa upande mwingine serikali inatakiwa kujikita katika utawala wa sheria kwa kutunga kanuni na taratibu za utendaji wake ambazo zinasisitiza uwazi na uwajibikaji wa viongozi kwa raia waliowachagua. Hivyo, changamoto ya ujenzi wa Demokrasia ni kusisitiza mambo yafuatayo:

(i) Kueweka kanuni, sheria na taratibu za utendaji zinazotilia mkazo uwazi na uwajibikaji wa viongozi wote wa serikali (kuhakikisha raia wanajua maamuzi muhimu ya serikali yanavyofikiwa, kuwafahamisha wananchi juu ya utekelezaji wa maamuzi na matokeo ya utekelezaji n.k.

(ii) Serikali sharti iwajibike kwa raia wake. Hivyo ni muhimu pawepo na kanuni na taratibu zinazosisitiza uwajibikaji e.g. katika ukusanyaji na utumiaji wa kodi za wananchi;

(iii) Viongozi wanaotuhumiwa na kuthibitishwa kuhusika na vitendo vinavyokiuka haki e.g. rushwa, kukiuka taratibu za kisheria zilizowekwa, wasingoje kufukuzwa bali wajiuzulu kulinda heshima ya serikali mbele ya wananchi;

(iv) Sheria lazima zitekelezwe kwa kuzingatia haki sawa kwa raia wote (watawala na watawaliwa). Yaani kusiwepo na tabaka la raia wa kuwajibishwa na sheria na wengine wakiwa juu ya sheria. Sheria, taratibu na kanuni zote ziheshimiwe na zitumike kuwabana raia wote bila upendeleo wa aina yoyote ile;

(v) Ushirikishwaji wa wananchi katika uaandaaji wa sera sharti uwekwe bayana. Pia kanuni na taratibu za ushirikishwaji hazina budi kuwekwa rasmi ili raia pamoja na viongozi wao waelewe namna watakavyoshiriki katika kuamua hatma yao.

- **Demokrasia na Maendeleo**

Demokarasia haina maana kwa watu wasiopata mahitaji muhimu, kama vile chakula cha kutosha, elimu bora, huduma bora za afya, maji safi ya kunywa na kupikia, na barabara za kusafirisha abiria na kusomba mazao. Kwa kifupi uchumi imara ndio unaoweza kuhakikisha kuwa Demokrasia inasitawi. Uchumi ambao hauhakikishi upatikanaji wa mahitaji muhimu huhatarisha Demokrasia kwa kuwa utaleta vurugu za kisiasa. Isitoshe watu wenye njaa ni rahisi kutumika kwa maslahi ya kisiasa ya watu wachache badala ya walio wengi.

Wananchi wataiheshimu na kuitetea serikali inayowajali. Serikali isiyojali hali ya kiuchumi ya raia wake hukosa imani na ridhaa ya watu wake. Hapa itabidi itawale kwa kutumia nguvu badala ya kuungwa mkono na raia. Hata hivyo, katika kuboresha hali ya maisha ya raia, ni muhimu raia wenyewe washirikishwe kwani wao ndiyo wanaojua ni kitu gani wanachokitaka kutoka serikalini. Ajira na mapato ni vitu ambavyo serikali haipaswi kuvidharau. Ni lazima wananchi wahakikishiwe vitu hivi sambamba na mahitaji muhimu. Hivyo Demokrasia haina budi kupiga vita umasikini wa kimawazo na umasikini kipato ili kumhakikishia rai maisha bora. Heshima ya raia inalindwa pale ambapo serikali yake haimnyanyasi bali inamhakikishia usalama wa mali, na usalama wa afya yake. Hatima ya yote ni raia kujisikia huru katika nchi yake na kuweza kutoa mchango wake katika ujenzi wa Demokrasia na katika ujenzi wa uchumi imara wenye kumhakikishia lishe bora, elimu bora na kadhalika.

- Demokrasia na Ushirikishwaji

Ushirikishwaji wa raia katika kufanya maamuzi muhimu ni utamaduni wa kisiasa unaotumiwa na raia katika kuleta mabadiliko ya kisiasa, kiuchumi na kiutamaduni. Yote haya yanalenga katika kuboresha maisha ya raia. Kimsingi raia hawaridhiki na maamuzi yanayofanywa na wawakilishi wao pekee. Kila wakati wanapenda kutoa mchango wao wa mawazo, na kama mchango huo wa mawazo hauheshimiwi na viongozi wa serikali hujiona wamedhalilishwa na kudharauliwa.

**Kwa nini ni muhimu kuwa na Demokrasia ya ushirikishwaji?**

Demokrasia ya ushirikishwaji ni muhimu katika kujenga taifa la raia wanaojiamini na kujisikia kuwa wao ni sehemu muhimu ya nguvu za kuleta maendeleo yao wenyewe. Pia imeonekana kuwa mara nyingi viongozi wanaochaguliwa, huwa na tabia ya kuwasahau na kuwadharau wale waliowachagua. Katika mikutano ya kampeni wagombea hutoa ahadi lukuki, ahadi ambazo huyeyuka mara baada ya matokea kutangazwa. Raia hujikuta wakisahaliwa na watu waliowachagua kwa kuwa wateule hawa hujihisi kwamba sasa wao ni viongozi waheshimiwa wa kusikilizwa tu na wapiga kura.

Ili Demokrasia iimarike hakuna budi raia washirikishwe na hasa wawezeshwe kufuatilia utendaji wa wale waliowachagua. Raia ni lazima wawezi kuhoji utendaji wa viongozi badala ya kungoja kuwawajibisha katika uchaguzi utakaofuatilia (kila baada ya miaka mitano). Hapa ni lazima raia wapate elimu ya uraia ili wapate upeo mkubwa wa kuhoji badala ya kupokea amri tu kutoka kwa 'waheshimiwa', viongozi waliosahau dhamana yao.Zipo njia nyingi za ushiriki.

(i) Ushiriki kupitia Vyama vya kiraia i.e. asasi mbalimbali za hiari;

(ii) Ushiriki kupitia vyama vya siasa

(iii) Ushiriki kupitia serikali za wananchi- ngazi za mitaa, vitongoji na vijiji.

Ushiriki wa raia kupitia asasi hizi ni muhimu kwa sababu zifuatazo:

(a) Kulinda maslahi ya makundi mbalimbali

(b) Asasi hizi huelimisha

(c) Kupunguza upweke wa kuachwa nje ya serikali na kuimarisha utetezi wa binafsi na ule wa matakwa ya jumuiya husika

(d) Kuhakikisha serikali na viongozi kwa ujumla wanawajibika hivyo kuhakisha utawala bora unazingatiwa na serikali

Inaposhindikana raia kushirikishwa katika kuamua hatima yao athari nyingi hujitokeza. Kwa mfano inaeleweka kwamba siyo rahisi kwa kila raia mmoja mmoja kuishinikiza serikali kuzingatia haki na kuwapatia raia maisha bora. Ni rahisi serikali kupuuzia raia mmoja mmoja lakini si rahisi kwa serikali kupuuzia nguvu na hoja za umma ulioungana kudai haki zao. Demokrasia huboreshwa na kukua pale raia wanaposhirikishwa kupitia asasi zilizo nje ya udhibiti na mwelekezo wa serikali. Watu wasiposhirikishwa uzalendo huwashinda na kujiona kwamba hawana dhamana wala faida kwa nchi yao. Watu wa namna hii ni rahisi kutimiwa na wapinga maendeleo na wale wasiopenda mwelekeo wa Demokrasia, hasa pale inapoelekea kuwamisha maslahi binafsi ya wale wenye uroho wa madaraka na mali.

Kwa ujumla, ushirikishwaji wa kidemokrasia huiwajibisha serikali kwa kuifanya ibuni na kutekeleza mbinu na mikakati ya kuandaa mipango na sera zenye kujali maslahi ya wananchi. Ieleweke kwamba ushiriki wa raia huboresha demokrasia. Pia kutoshirikishwa raia hudumaza demokrasia kwa kuwa mawasiano kati ya wananchi na serikali yao hukatika. Kukatika kwa mawasiliano kati ya watawala na watawaliwa ni hatari kwa kuwa hupelekea raia kujichukulia sheria mkononi kwa kujua kwamba serikali imeenda likizo au imewapuuza na hivyo kuamua kujifanyia lile walitakalo wao. Utawala wa sheria hudumaa na demokrasia huvia inapotokea hali ambayo raia na serikali kila mmoja anajifanyia apendavyo bila ya mashirikiano yaliyoboreshwa na kanuni na taratibu za kiungwana. Yaani taratibu zilizotengenezwa kwa makubaliano kati ya watawala na watawaliwa ndicho kigezo muhimu katika mkataba hiari wa utawala.

Ushiriki wa raia katika ujenzi wa uchumi imara na demokrasia thabiti unaweza kuchukua sura mbalimbali. Kiondo (1997) ameelezea njia mbalimbali kama ifuatavyo:

1. Kujielimisha mwenyewe katika mambo mbalimbali yanayohusu jamii, uchumi, siasa pamoja na uongozi.
2. Kuelimisha wengine kwenye mambo yote hayo hayo.
3. Kuhamasisha jamii ili kuiunga mkono serikali katika juhudi za kuboresha maisha ya jamii.
4. Kuunda na kujiunga na vyama vya siasa na vile vya kijamii.
5. Kuhudhuria mikutano ya siasa pamoja na ile inayoandaliwa na jumuiya.
6. Kushiriki katika uchaguzi wa viongozi wa kisiasa – katika chama au katika asasi nyingine ya kijamii.
7. Kushiriki katika kupiga kura kwenye uchaguzi mkuu kuchaguz viongozi wa serikali kitaifa.
8. Kufanya kampeni kwa niaba ya wagombea.
9. Kugombea uongozi na kuwa tayari kutumikia nafasi kama ukichaguliwa.
10. Kuheshimu haki za wengine.

**Hitimisho**

Hakuna maendeleo yoyote yanayoweza kupatikana bila kuweponademokrasia. Pia hakuna demokrasia bila ya kuwashirikisha raia. Wananchi wanataka maisha bora, na ili maisha yawe bora hakuna budi kuwashirikisha katika kufikia maamuzi yanayogusa maslahi yao. Wananchi wanaweza kushirikishwa kupitia vyama vya siasa au kupitia asasi huru za kiraia. Faida kubwa ya ushirikishwaji wa raia ni kuhakikisha serikali inafuata utawala wa sheria na pia kuhakikisha matakwa ya raia yanasikilizwa na kutekelezwa.